

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI YA HUDUMA ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MJI WA MAKAMBAKO (“MAKAMBAKO WSSA”) KWA MWAKA 2018/19 – 2021/22

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-029-2018

Mnamo tarehe 7 Februari 2019, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Makambako (Makambako WSSA) la kutaka kurekebisha bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2018/19 hadi 2021/22. Jedwali namba 1 hadi 3 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Maji za sasa na zinazopendekezwa (shilingi kwa mita moja ya ujazo)

Aina za Mteja	Bei za Sasa	Bei zilizopendekezwa							
		2018/19		2020/21		2021/22			
		% Badiliko	2018/19	% Badiliko	2020/21	% Badiliko	2021/22		
Majumbani	580	85%	1,071	6%	1,140	11%	1,269	12%	1,422
Taasisi	730	84%	1,344	6%	1,431	11%	1,592	12%	1,784
Biashara	745	85%	1,376	7%	1,466	11%	1,631	12%	1,828
Viwandani	1045	84%	1,923	7%	2,048	11%	2,279	12%	2,553
Magati	500	118%	1,092	7%	1,164	11%	1,295	12%	1,451
Ujenzi	1,460	84%	2,687	7%	2,862	11%	3,185	12%	3,568

Jedwali 2: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya (Shilingi kwa maunganisho mapya)

Aina za Wateja	Bei za Sasa		Tozo zilizopendekezwa						
	2018/19	% Badiliko	2018/19	% Badiliko	2019/20	% Badiliko	2020/21	% Badiliko	2021/22
Majumbani	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa
Taasisi									
Biashara									
Viwandani									
Magati									
Ujenzi									

Jedwali 3: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshwa Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwa marejesho)

Customer category	Bei za Sasa	Bei zilizopendekezwa							
	2018/19	% Badiliko	2018/19	% Badiliko	2019/20	% Badiliko	2020/21	% Badiliko	2021/22
Majumbani	16,000	25%	20,000	25%	25,000	20%	30,000	17%	35,000
Biashara	22,000	36%	30,000	17%	35,000	14%	40,000	13%	45,000
Taasisi	22,000	36%	30,000	17%	35,000	14%	40,000	13%	45,000
Magati	22,000	36%	30,000	17%	35,000	14%	40,000	13%	45,000
Ujenzi	22,000	36%	30,000	17%	35,000	14%	40,000	13%	45,000
Viwandani	22,000	36%	30,000	17%	35,000	14%	40,000	13%	45,000

Kwa mujibu wa wasilisho la Makambako WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kupata mapato ili kumudu gharama halisi za uendeshaji. Mamlaka ya maji Makambako wamebainisha kuwa mabadiliko ya bei na tozo yanayopendekezwa yataiwezesha Mamlaka kumudu gharama za uendeshaji zilizoongezeka, kuboresha huduma za maji safi ikiwa ni pamoja na kuongeza mtandao wa majisafi na kufanya uwekezaji wa miundombinu ya maji ili kuboresha utoaji wa huduma ya maji safi katika mji wa Makambako.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 11 Aprili 2019, katika Ukumbi wa Green City, Mjini Makambako** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu ndani ya kipindi kabla ya tarehe **18 Aprili 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Ofisi za UWURA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, **GHOROFA YA SITA, JENGO LA NHIF, MTAA WA KARUME, S.L.P 2245 MBEYA** au Ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mji wa **MAKAMBAKO** zilizopo Mkabala na Barabara ya Songea.

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
15 Machi 2019